

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI

05 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 05 JUNI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

516. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini barabara ya Irambo - Nsonyanga inayounganisha barabara ya Isyonje - Makete hadi Njombe na Tanzam itapandishwa hadhi.

517. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Getifonga – Mabogini hadi Kahe.

518. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwalo la Shule ya Sekondari Igwachanya - Njombe.

519. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwezesha Shule za Kata kuwa pia za Kidato cha Tano na Sita kutokana na kuongezeka kwa ufaulu.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

520. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Viongozi Wastaafu wa Vitongoji na Vijiji wenye sifa sio wanufaika wa *TASAF*.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

521. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, miaka 5 iliyopita Tanzania ilipata kiasi gani kutoka Mfuko wa Fedha za Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Mataifa.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

522. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Minara ya Simu itajengwa Endahagichang Tunati Jing, Qalodaginwe, Aidurdagawa, Qamtananat na Migwa.

WIZARA YA AFYA:

523. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza huduma za afya na dawa zinazotolewa kwa Bima katika Zahanati na Vituo vya Afya.

WIZARA YA NISHATI:

524. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapitia upya malipo ya umeme Vijiji vya Mkolango, Kiumba, Ikwete na Malombwe ambao walilipia kwa bei ya Mjini.

525. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Vijiji vyote vya Mkoa wa Songwe vinapatiwa umeme wa REA.

WIZARA YA KILIMO:

526. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Skimu ya Umwagiliaji katika Kijiji cha Mtitaa Wilayani Bahi.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

527. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itatoa ithibati kwa baadhi ya Pombe za Kienyeji ambazo zimekidhi viwango.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

528. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango wa ujenzi wa Vizimba vya Ufugaji Samaki katika Ziwa Duluti.

529. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itamalizia fedha za ujenzi wa Soko la Samaki Bagamoyo.

530. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna utaratibu gani umewekwa kuwapatia mikopo Wavuvi wadogo wa upande wa Zanzibar.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
05 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

